

UTAMADUNI WA MWAFRIKA KATIKA RIWAYA YA BWANA MYOMBEKERE NA BIBI BUGONOKA

S.A.K. Mlacha

Utangulizi

Riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka* ni mojawapo ya riwaya ambazo zimezingatia utamaduni wa Mwfrika. Utamaduni ambao umepitia tawala mbalimbali kama vile utawala wa Waarabu, Wajerumani na Waingereza, Wafaransa na wengineo katika bara letu hili. Tawala hizo ziliweza kupenyeza tamaduni zao (Mlacha 1987) na kuathiri kwa kiasi kikubwa mawazo na hata matendo ya Waafrika. Elimu na dini zilitumika kwa muda mrefu ili kufifisha utamaduni wa Mwfrika. Kwao, kama asemavyo Sengo na Lucas (1975:6):

Mila na desturi zetu hazikuwa za kiungwana,
Mwfrika aliyebaki akifanya ya Kiafrika alionekana
mshenzi na mtu asiyeedelea.

Mawazo ya aina hii yamejitekeza kwenye baadhi ya kazi kadhaa ambazo hazikuangalia utamaduni wa Mwfrika kwa kumwangalia Mwfrika na maisha yake. Kazi za wataalamu kama vile Knappert (1979) zinatoa taswira ya utamaduni duni wa Mwfrika. Katika uchambuzi wake wa tenzi za Kiswahili anaonyesha jinsi utamaduni wa Kiarabu ulivyo bora na jinsi ambavyo sifa nzuri za maisha ya Mwfrika zilivyotokana na sifa nzuri za utamaduni wa Kiarabu. Aidha, anadai kuwa amali nyingi za utamaduni wa pwani ya Afrika Mashariki zilikuzwa, kuhifadhiwa na kuendelezwa na Waarabu na Wazungu ambao utawala wao uliongozwa na utamaduni bora (Knappert hasa 1979:62). Hata hivyo, wapo wataalamu ambao waliweza kuutetea utamaduni wa Mwfrika (Mbiti 1969; Mlacha 1987) na hata kuonyesha jinsi Mwfrika alivyothamini utamaduni wake katika kuendeleza shughuli zake za kila siku. Ni katika kutetea utamaduni wake ambapo Mwfrika amejikuta katika mapambano makali.

Makala haya yanazingatia jinsi kazi ya kisanii iliyoandikwa na Kitereza ilivyoweza kutunza mila na desturi za kabile mojawapo hapa Tanzania. Riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka* itachambuliwa hapa kwa nia ya kuonyesha jinsi msanii alivyofanikiwa kuzionyesha mila na desturi za Wakerewe na kuzirithisha kutoka kizazi hadi kizazi. Tofauti na wataalamu wengine ambao wameeleza "kwa muhtasari dhamira muhimu bila uchambuzi" (Madumulla 1988) au ambao wametoa ufanuzi kwa kugusia kipengee kimojakimoja tofauti (Mulokozi 1985; Hartwig na Charlotte 1972), makala haya yatachambua vipengee muhimu vilivyojitekeza.

Uchambuzi huu umeelekezwa kwenye kabile moja la Watanzania ambao wamebeba utamaduni mmoja ikiwa ni njia mojawapo ya kuanzisha uchunguzi

mkubwa zaidi utakaojumuisha utamaduni wa makabila mengi zaidi na kulinganisha tamaduni tofauti baina ya makabila hayo. Nia nyingine ya makala haya ni kuonyesha kwamba uchambuzi wa riwaya, na hasa riwaya za historia za maisha, unaweza kuwa njia ya uchunguzi wa sanaa ya jadi pamoja na kutumiwa katika ukuzaji na usambazaji wa utamaduni nje ya mipaka ya kabilia moja. Wataalamu kama vile Langness (1965) na Pentikainen (1976) wameweza kutumia kumbukumbu na hadithi za maisha ya watu katika uchunguzi wao na kuweza kugundua historia ya makundi tofauti ya jamii za Finland.

Kuna kazi kadhaa zilizozingatia na kuhifadhi utamaduni wa jamii za Afrika Mashariki. Kitabu cha Kitereza ni kati ya kazi ambazo zimezingatia sana suala hili. Mwandishi amechukua jukumu kubwa kwa niaba ya watu wa jamii yake (labda bila yeche mwenyewe kunuia hivyo) katika kuuhifadhi utamaduni wa Wakerewe tokea mwaka 1945 hadi hivi leo. Ili kutorudia yale yaliyojadiliwa na Mulokozi (1985) na Madumulla (1988) hatutarudia maudhui ya riwaya hii.

Muundo wa riwaya

Riwaya hii imeandikwa katika muundo ambao ni muhimu sana kwenye kuelezea muktadha wa utamaduni wa watu. Muundo huu, ambao unaonyesha uhusiano baina ya mtu, utamaduni unaomzunguka na muundo wa jamii unaothibitisha kwamba mtu si sehemu tu ya jamii yake bali pia ni sehemu muhimu katika kuikamilisha jamii hiyo. Hivyo matendo na imani zake ni sehemu ya matendo na imani za jamii na pia matendo na imani za jamii yake yanajumuisha matendo na imani zake. Uhusiano huu wa kimzunguko ni muhimu hasa tukiangalia kuwa mtu anazaliwa na kuingia kwenye jamii yenye utamaduni maalum ambao una muundo kamili. Muundo huu unaruhusu nafasi ya mtu huyo kuwa na nafasi maalum katika jamii hiyo muda wote wa maisha yake. Kwa mfano, Myombekere anakuwa mtoto, mume, baba na hata babu, mjomba, shemeji na kadhalika. Bugonoka naye anakuwa mtoto, mke, mama, shangazi na kadhalika kulingana na upana wa mahusiano ya kijamii. Katika uhusiano mpana wa utamaduni wetu, Myombekere na Bugonoka, kama mume na mke, wana wazazi wao ambao jamii inawadai wawasikilize na kuwatii. Wapo majirani na ndugu ambao wanachangia sana kuwepo na kutokuwepo kwa watu hao kama wanajamii. Wao wenye hawawezi kuikana nafasi hiyo na bado katika kuishi kwao wanaitegemea sana jamii hiyo. Uhustiano wao na kila mwanajamii ndio unaonyesha na kuithibitisha nafasi yao ndani ya jamii.

Nje ya mzunguko huo wa mtu, utamaduni unaomzunguka na muundo wa jamii na mtu, upo mzunguko mwingine unaomtawala mtu ndani ya jamii, ambao huthibitisha utamaduni huo na kuuimarisha muundo wa jamii. Mzunguko huu ni ule wa mila na desturi ambao unaifanya jamii moja kuwa tofauti na nyingine. Hata hivyo uhusiano baina ya mzunguko huu na ule wa mtu, utamaduni na muundo ni wa kutegemeana. Mtu anatawaliwa na mila na desturi wakati mila na desturi zinategemea kuwepo watu ambao wanazifuata. Utamaduni unakamilika kukiwepo na mila na desturi wakati mila na desturi nazo zinajengeta kunapokuwa na

utamaduni unaoelewaka. Kadhalika muundo wa jamii una uhusiano huohuo wa kutegemeana na mila na desturi. Ni kipi kinachoanza? Ili kujibu swali hili inahitaji uchunguzi wa kianthropolojia na sanaa ya jadi na ni mada ambayo sitaijadili hapa.

Katika Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka itaonekana kuwa Myombekere anaweza kukiuka aina fulani za utamaduni wake na hata muundo wa jamii lakini inapofikia kwenye mila na desturi uwezo huo unaonekana hanao. Kwa mfano ingawa anakiuka uamuvi wa wazazi wake kuhusu kuishi na Bugonoka kama mke (kwa kwenda kuomba msamaha kwa wakwe zake na kupewa mke wake), mke ambaye wazazi wake wameona hafai kwa vile hazai, inapofikia mila na desturi anakwama. Kwa mfano anapokutana na mwanamke mmoja njiani na kuanza kumposa anatambua kwamba mila na desturi zao haziwaruhusu wao kuoana. Pamoja na nia yake kubwa ya kuo, Myombekere anaamua kuacha wazo lake.

Mila na desturi katika Bwana Myombekere

Kutokana na riwaya hii ambayo ndiyo chimbuko la uchunguzi huu, taarifa hizi za miaka 43 tunaweza kuzitumia ili kuonyesha kwamba riwaya hii inafaa isomwe katika muktadha wa maisha, mila na desturi za Kitanzania ili kufanikisha lengo la kukuza utamaduni wetu, kwani kama alivyosema Pentikainen (1976:271)

wakati zinapotolewa suala muhimu sio tu kuzitunza mila na desturi hizo alizojifunza mwelezaji, bali pia kuziendeleza na kuzikuza.

Katika riwaya zake, Anicet Kitereza ameweza kumtumia mhusika wake mkuu, Bwana Myombekere, na pia Bibi Bugonoka, kuonyesha mila na desturi za Wakerewe katika maisha yao ya kila siku. Mulokozi (1985:213) anaeleza wazi kwamba lengo kuu la Kitereza lilikuwa ni kutunza lugha, mila, desturi na utamaduni wa Bakerewe. Mulokozi alibahatika kuongea na mwandishi huyu na zaidi ya hayo ameshughulika sana katika kukitoa kitabu hiki kiasi ambacho tunaweza kusema uhusiano wake kikazi na Kitereza umempa uwezo wa kusema hayo kwa pande mbili. Kwanza kutokana na kauli za Kitereza mwenyewe na pili kutokana na riwaya yenye. Kwa kutumia kisa cha kusikitisha, kisa kilichosababishwa na desturi za kabilo hilo kwamba mwanamke asiyezaa anastahili kuachwa na mumewe, kwamba uzazi ndio ishara ya kukuza ukoo, mwandishi ametupitisha kwenye raha na taabu, uzuri na ubaya wa kufuata mila na desturi. Mwandishi ameweza pia katuonyesha kuwa Myombekere ameletelewa na jamii chini ya misingi hiyo ya mila na desturi na kustahili kuangaliwa kama mtu mwenye sifa pekee, maisha na tabia yake maalum na pia kama mjambe wa kikundi cha jamii katika mazingira ya utamaduni wake. Namna anavyotekeleza mila na desturi za jamii yake ndivyo ambavyo anaimarisha uhusiano baina yake na wanajamii wengine. Katika hali hiyo ya inawasiliano na uhusiano wao ndipo tunapoweza kuona maarifa na ujuzi wa pamoja, matumaini na mategemeo ya pamoja. Kwa mfano mkewe anapotafutiwa waganga wa kumtibu. Waganga wanatumia ujuzi wao

na baadaye mkewe anafanikiwa kupata mtoto, na hadhi ya Myombekere katika jamii inabadilika. Katika uhusiano huo tunaona kwamba sifa za Myombekere kama mtu na zile za idadi kubwa ya watu wa jamii yake ndizo zinazotupa taswira ya aina ya sifa za mawazo na matendo ya jamii (wakarimu, wanaheshimiana, wana mawazo ambayo hayatofautiani sana katika shughuli zao za kila siku na kadhalika). Sifa hizi ndizo zinazoweza kulinganishwa na sifa za jamii nyingine na kujenga sifa za pamoja kwa upana zaidi.

Lakini kabla hatujaendelea zaidi ni muhimu kuelezea maana ya mila na desturi kama tutakavyoitumia katika makala haya. Anaclet na wenzake (1979:2) wameangalia mila kama:

Hali ya kudumu ya maisha ya kila siku
ya watu ambayo inahusu sana asili ya watu
na hivyo kupokezwa kutoka kizazi hadi kizazi na kuthaminiwa sana na
watu kama dira ya maisha yote ya kijamii.

Wanaendelea na kuelezea kwamba mila hujumuisha malezi na huonekana katika miiko, historia, matibabu, heshima na kadhalika. Kuhusu desturi wanasema kuwa ni mazoea ya jamii katika muhula maalum wa historia. Ben-Amos (1976:35) naye anasema kwamba mila huchukua nafasi muhimu na iliyomakinika katika mahusiano ya kijamii. Malinowski (1973) anasisitiza kuwa tanzu hizi ni sehemu ya utamaduni na hapohapo huujenga utamaduni. Kama tanzu zingine, Malinowski anaongezea, tanzu za mila na desturi zina mchango mkubwa katika kutunza na kuendeleza utamaduni wa kijamii. Maelezo haya yote yanaweza kutosheleza kile tunachoongelea hapa.

Utunzaji na Usambazaji wa Mila na Desturi

Utunzaji na usambazaji wa mila na desturi unaweza kufanyika kwa njia nyingi na kwa viwango tofauti. Njia hizo zinaweza kuwa kwa mapokezi ya mdomo au kwa maandishi. Aidha kuna njia ya vifaa maalum vya matumizi ya kila siku au vyakula. Utunzaji na usambazaji huo unaweza kuwa kwenye kiwango cha familia moja, kama vile familia ya wahanzi; kwa jamii moja au hata baina ya jamii moja na nyingine. Washiriki katika utunzaji na usambazaji huu ni wanajamii wote lakini kuna wale ambaovon Sydow (1948) aliwaita "wasambazaji na watunzaji wa mila na desturi kibiolojia". Hawa ni wale watu katika jamii ambaovon ni watendaji. Ni kama vile wazee ambaovon wamemakinika katika utunzaji na usambazaji huo na wana uwezo (kutokana na muundo wa jamii) wa kuzipokea mila na desturi hizo toka kizazi kimoja hadi kingine. Watu kama hawa ni pamoja na waandishi kama Kitereza. Sydow anasema pia kuwa wapo wale watu ambaovon sio watendaji. Hawa ni wale ambaovon hawafanyi jittihada maalum kutunza na kusambaza mila na desturi zao. Watu wa aina hii ni kama vile Myombekere, na hata Bugonoka, ambaovon wanaishi chini ya mila na desturi zao na ni matendo yao yanayoweza kuigwa na wengine bila wao kujua. Kwa mfano Myombekere anapojitahidi kutomwangalia

mkwe wake hii ni kwa sababu anazielewa mila na desturi zake. Sio kwamba anafanya hivyo kwa makusudi ili mtu mwingine aweze kutenda hivyo. Kitendo chake kinatuonyesha kwamba ni mtekelezaji. Nadharia ya von Sydow inaweza kuchambuliwa kwa upana zaidi hasa kuhusu mipaka yake, kasoro zake na umuhimu wake katika kusambaza mila na desturi za Kiafrika. Si lengo la makala haya kuichambua nadharia hiyo kwa upana kwani suala hilo limejitokeza kwenye makala nyingine (Mlacha 1996).

Tukianza na Kitereza mwenyewe tunaweza kusema kwamba, kama mtunzaji na msambazaji anayetenda, amechukua vitendo maalum vya utamaduni wake na kuviweka katika maandishi kwa faida ya watu wote wa wakati wake na wakati ujao. Amezingatia tanzu zote za utamaduni wake na pia shughuli za kila siku katika jamii yake ili kuitoa taswira maridhawa ya jamii hiyo. Kila utanzu umeangaliwa kwa ujumla kuhusiana na muundo wa utamaduni wa jamii kama kitu kimoja. Kwa hivyo mila, desturi, lugha, vyombo, sherehe, nyimbo, methali na kadhalika vinakuwa ni sehemu muhimu ya maelezo yake. Alichofaya Kitereza ni kuchukua yote haya na kuyapitisha kwa "wahusika hai" ili kuipa hifadhi yake uzito. Mtindo huu ulianza zamani sana na hasa mnamo karne ya 19 wakati ambapo Grim na wenzake huko Ujerumani walipoandika hadithi zao. Kitereza amemtumia Bwana Myombekere kama mwanajamii ambaye si bingwa sana katika mila na desturi za jamii yake lakini mwenye kuweza kutekeleza mengi ya yale yanayotarajiwa kwake na jamii. Kwa vile yeye si mtendaji thabiti ana uhuru wa kukiuka vipengee vingine ili kutimiza mahitaji na matakwa yake binafsi, hasa kunapokuwa na mgongano baina ya matakwa na mategemo yake dhidi ya matakwa na mategemo yake jamii. Ndio maana tunamwona akikiuka uamuzi wa wazazi wake kwamba lazima aachane na Bugonoka kabisa. Inapofikia mkewe kuwa kwenye hatari ya kuumwa na nyoka yeye yupo tayari kwenda kumuua nyoka yule akiwa amesahau mila na desturi zake. Yeye na mkewe wanapobishana juu ya kumuua nyoka huyo mkubwa mkewe anamstua kwa kumkumbusha kosa ambalo analifanya:

ehem, umekuwa mwehu leo?
Uue nyoka kweli? Na wewe
mtu mzima hivi useme: niue nyoka
Au labda kwa kuwa huzai.....
wewe huogopi kupata balaa kwa siku
za usoni? (uk. 144)

Katika hali hii Bugonoka anakuwa bingwa wa kuikumbuka na kuiendeleza mila hii inayomhusisha nyoka na mambo yatakayotokea baadaye. Imani yake hiyo inaungwa mkono na mwanamke mzee na hata Myombekere anakiri "siwezi kamwe kuvunja kanuni ya watu wote" (uk. 145). Hapa inaonyesha kuwa mila na desturi zilizopo zimekitwa kwenye imani na pia kuwa na muktadha maalum ambao unaeleweka kwa wanajamii. Kufuatana na muundo wa jamii hiyo mtu mzima kama

Myombekere alitarajiwa awe anajua kwamba kuvunja imani hiyo kungemletea balaa. Ni mtoto tu ambaye anastahili kufahamishwa haya, kama alivyoashiria Bugonoka. Baada ya kukumbushwa yote hayo Myombekere anatupilia mbali wazo lake la awali na kujifanya alikuwa anatania tu. Hata hivyo anarudia tena kosa hilohilo baadaye, wakati anapomwona nyoka mdogo karibu na kitanda cha Bugonoka na Ntulanalwo (mtoto wao). Anapotaka kumpiga yule nyoka mama mkwe wake anatokea na kumzuia akisema:

Acha mwanangu usikiue, ni mwiko.
Je wewe unajua kisa kilichomleta
nyoka huyu, kisha hii si nyoka
kama nyoka wengine tunaowaona; ni
ya mizimu, mke wako mwambie
akupe maji, utie mdomoni mwako
halafu uteme (uk. 331).

Hii inaonyesha jinsi ambavyo Myombekere alikuwa hajui mambo mengi. Vilevile inafafanua kwa nini mwiko huu katika mila zao umemstua mama mkwe alipoona kuwa Myombekere alitaka kumuua nyoka yule.

Mojawapo ya mila na desturi zinazojitokeza sana katika kitabu cha Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka ni yale mambo ambayo wanajamii wanatakiwa kufanya kwa faida ya maisha yao au jamii nzima. Mwanzoni mwa kitabu Aniceti Kitereza anaonekana akisisitiza zaidi uhusiano baina ya wakwe. Uhusiano huu inaonyeshwa kama wa kuepana na kuogopana. Watu hawa wawili hawapaswi kuonana uso kwa uso na huenda mojawapo ya sababu ni kutunza heshima baina yao. Mwandishi anatueleza kinaganaga na kufafanua anaposema:

Nkanzi akamwambia mkwe wake,
"Jitenge, mkwe wangu, niingie
ndani." Mkwe wake akajitenga
na kugeuza uso wake upande mwininge
wasionane uso kwa uso, kwa kufuata
mila ya watu. (uk 12).

Tukiangalia maelezo haya tutaona kuwa katika mila hiyo kuna uhusiano wa mtu na mkwe wake katika mfumo wa jamii. Anaendelea kusositiza heshima hii iwapo tutarudi nyuma na kuona anaposema:

Alipofika karibu na mlango akajibaza
ukutani kwa adabu ya mila ya nchi,
ili asipate kuonana mama mkwe
wake uso kwa uso na. Hapo akapiga
mafuti akijikinga upande wa mkono

wa kushoto, sababu alijua upande
aliyokuwamo mama mkwe wake... (uk. 5).

Uhusiano huu umetengwa kwa kutumia kipengele cha heshima ambayo inamkumbusha mkwe kuitambua nafasi yake kila akutanapo na mwewewe. Heshima baina ya wakwe ina uhusiano na utamaduni wa jamii pamoja na muundo wa jamii. Wakwe wanajitambua nafasi zao katika jamii na baina yao na hivyo kupeana heshima kulingana na mila na desturi zao. Heshima baina yao nayo inaweza kuzaa heshima baina ya watu wa jamii moja au hata jamii moja na nyine hasa kwa vile watu wanaweza kuoana katika jamii hiyo hiyo kama alivyofanya Myombekere au katika jamii nyine kabisa kama inavyokuwa kawaida siku hizi.

Mwandishi anaposimulia Myombekere anavyotimiza mila na desturi za Wakerewe anaelezea pia kuwa zipo mila na desturi ambazo zinahusu wageni. Mila hizi zinaonyesha kuwa watu hawa wana ukarimu mkubwa na mila na desturi zao hazimpi mtu nafasi rahisi ya kuzikwepa bila sababu maalum. Kwa mfano mgeni anapofika mahali anapewa fursa ya kujisikia yupo nyumbani, pamoja na watu wake, hasa kwa vile hazimruhusu mtu huyo kukataa kujiunga na wenyeji wake katika shughuli inayoendelea wakati huo. Pamoja na mifano mingine inayohusu mapokezi na kusindikizana, mwandishi ametoa mfano wa mgeni anapokuta watu wanakula. Kitereza anasema:

Lakini kuamkiana, hapana,
kwa sababu aliwakuta wanakula
na ndiyo hiyo ilikuwa kanuni
ya mila ya nchini Bukerebe (uk 125).

Mila hii inaweza kuwa imetokana na sababu nyine lakini mojawapo ambayo inaweza kuelezwu kutokana na riwaya hii ni ile inayoweza kuhusishwa na shughuli za watu hao. Shughuli ya uvuvi ni mojawapo ya kazi zao muhimu hasa wakiwa ni watu wa ziwani. Hivyo, ingawa haikufafanuliwa hivyo, inawezekana kwamba kwa vile samaki ni mlo wao mkubwa kutoongea na watu wakati wanakula kunaweza kuwa ni kuwaepusha wasije wakaathiriwa na miba ya samaki kwa kula huku wanaongea na mgeni. Lakini jambo la muhimu zaidi hapa ni kwamba mgeni anakaribishwa moja kwa moja kuhusika kwenye kula chakula kwa kufuata mila na desturi za jamii. Hii inaonyesha kwamba jamii hiyo haitoi nafasi kwa watu wachoyo. Ukichanganya na namna ya mapokezi na usindikizaji inaonyesha jinsi watu hawa walivyokuwa wanawapa wageni heshima kubwa.

Pamoja na mila na desturi hizo ambazo Kitereza ameziona ni muhimu sana na zinahitaji kuendelezwa na kuzingatiwa, zipo mila na desturi nyine ambazo anaonelea zina walakini. Amejaribu kuzigusia ili kuonyesha kwamba hata ndani ya utamaduni wa jamii viro vitu ambavyo vinastahili kuangaliwa kwa jicho lingine na kwamba sio wanajamii wote wanaviunga mkono. Mojawapo ya mambo haya ni lile ambalo limeizaa hadithi hii. Kupata mtoto katika familia ni kitu ambacho

Kitereza ameonyesha kwamba ni muhimu. Hata hivyo, riwaya yote hii inaonyesha kwamba alichotaka kuonyesha ni kwamba mtu kutopata mtoto si mwisho wa maisha na wala haina uhusiano wowote na uwezo wake kama mtu. Pamoja na kwamba Kitereza leo hii anaonekana nyuma ya wakati kwani watu wanaweza kupata watoto nje ya uwezo wao wa kibiolojia na pia wanaweza kushindwa kupata watoto kwa sababu zao wenyewe au matendo yao, kulingana na hadithi hii wazazi wa Myombekere waliamini kwamba Bugonoka alikuwa anastahili lawama na ndiye aliyemnyima mtoto wao watoto. Kitereza anaelekea kuwa na mawazo mchanganyiko. Hayo ni mawazo ya kuamini yale wanayoyaamini wazazi wake Myombekere ambayo wengi, pamoja na Kitereza, wanaelekea kututilia maanani sana. Mengine ni mawazo ya kuamini waganga na nguvu za Mwenyezi Mungu. Katika mjadala huu inaelekea wazo la kumshutumu Bugonoka kwa kutozaa na kumfanya aachane na mumewe limeonyeshwa kama wazo baya ambalo linastahili litupiliwe mbali. Aidha anaelekea kupinga wazo la wazazi kuingilia ndoa ya watoto wao hasa inapofikia maamuzi ya maisha yao. Hata hivyo Myombekere alijikuta kwenye taabu kubwa kabla hajaweza kufanikiwa katika malengo yake. Mwandishi anashutumu usisitizaji wa mahari bila kujali maisha ya watu hao wanaohusika. Anayasema haya kuititia kwa mwanamke anayesema:

Ati yule alikosa kunipa
mahari, basi baba yangu akaja
kunitoa kwa nguvu, nikaenda
kwetu na kitoto mgongoni kina-
nyonya (uk 216).

Hii inaonyesha kuwa Kitereza hakubaliani na kila mila na desturi ya watu wake na kwamba sio mila na desturi zote zinakubaliwa na watu wa jamii hiyo, ingawa hawawezi kuepa kuathirika.

Mtu, mila na desturi

Kitabu cha Kitereza kinaelekea kujibu swali moja muhimu katika kuueleza uhusiano baina ya mtu, mila na desturi zake. Swali hili ni muhimu kwa vile ndilo ambalo linazingatia dhamira zinazojitokeza katika kitabu hiki. Swali hili limejibiwa kuititia kwa Myombekere ambaye ameingizwa ndani ya jamii ambayo ina muundo wa kumiliki mtoto. Wazazi wanayo nafasi kubwa katika kumwamuru mtoto atende yale wanayodhani ni sawa na mtoto hana uhuru kamili kuamua vinginevyo. Japo Myombekere ni mtu mzima, anapambana na mawazo ya wazazi wake kwa tabu mno. Uamuzi wa wazazi wa mke unakuwa mzito zaidi na hana njia ya kuipinga. Mkewe naye inabidi akubaliane na wazazi wake. Kufuatana na mila na desturi za jamii Myombekere na Bugonoka wanawajibika kukubaliana na maamuzi hayo ya kimila kuititia kwenye muundo wa kijamii, kulingana na uhusiano wa wazazi na watoto. Wazazi wa Myombekere nao wametawaliwa na mila na desturi zao katika imani ya kuwa mwanamke asiyepata mtoto hastahili kuishi na mume' kwani suala

la kukuza ukoo linakuwa mbele. Mtu huzaliwa ili azae. Nafasi ya Myombekere kutafakari juu ya kukubaliana au kutokukubaliana na uamuzi huo inakuwepo hasa kwa vile imani ya wazazi wake ni imani ambayo hajakubalika kikamilifu katika jamii, kama asemavyo Nenola-Kallio (1986:108-9) kuwa mila na desturi huingizwa kichwani mwa mtu hadi anapozikubali kama ni sehemu ya maisha yake. Hivyo desturi za wazazi wake hazijamuingia kikamilifu kichwani mwake.

Myombekere anaingizwa ndani ya mila na desturi za jamii yake kwa hali tofauti za kiuhusiano ambazo ndizo zinazomjenga na kuunda sifa zake. Kati ya hali hizo tutaangalia hali tatu kwa ufupi. Hali ya kwanza ni ile inayotokana na muundo wa jamii yake kama tulivyogusia juu. Jamii yake inaundwa katika matabaka ya mtoto, wazazi, ndugu na jamaa wengine wanaozunguka familia yake. Muundo huu una maisha ambayo Myombekere anatarajiwa aishi hivyo na anawategemea watu wote hawa kwa ushauri na msaada. Anapokwenda kuomba msamaha kwa wakwe zake anawatafuta ndugu na majirani ili wamsindikize ikiwa ni sehemu ya mila na desturi zao. Mtoto wake anapouguwa anawauliza watu ili kupata ushauri na ndugu yake, ambaye ndiye mkubwa katika ukoo wao, anampa ushauri wa kimila:

Omba dua kwa Mizimu upesi,
watu wachinje mbuzi; shika mkuki
wako uitwao nabuhotora katika
mkono wako wa kushoto... (uk 134).

Kwa hali hii Myombekere anaeweshwa mila na desturi zake kwa kufanywa ajihusise moja kwa moja. Pamoja na kupata ujuzi anaitambua nafasi yake na majukumu yake kama mwanajamii. Hali ya pili ni ile inayotokana na watu na mabingwa wa mila na desturi za jamii yake. Watu hawa wanachukua jukumu la kumuingiza Myombekere katika mila na desturi kwa kumfunza na kumkumbusha. Kwa mfano wakati anapozaliwa Ntulanalwo, Myombekere alikuwa hajui mambo mengi. Mwandishi anasema:

Basi kwa sababu Myombekere alikuwa
hajajua jinsi wanavyosema watu kwa
kumpa mtoto jina alianza kuauliza
wakamfahamisha.....(uk 311).

Kutokana na hali hiyo Myombekere anaendelea kujifunza mambo mengi ambayo yanahuus mila na desturi ambazo alikuwa hazifahamu. Waganga wa mvua na wa magonjwa na hata viongozi wa kimila kama vile watemi wanakuwa na athari kubwa katika kumfanya awe mshiriki katika jamii. Myombekere anaingizwa ndani ya mila na desturi kutokana na njia nyininge ambayo ni ya utekelezaji wa mila hizo. Njia hizo ni pamoja na shughuli za kila siku kama vile ufugaji, uvuvi, ukulima na kadhalika. Kwa mfano Bugonoka anapotakiwa kumshughulikia mtoto wake mchanga mwandishi anasema:

Bugonoka alikuwa amekwisha kusimama
na kutoka pale alipozalia na yeze
aliakuwa anaangalia ufundi wa kukata
kile kitu cha kitovu cha mtoto wake
.....(uk. 30).

Hali hizi zote ambazo ni matokeo ya elimu na malezi katika jamii humpatia mwanajamii kama Myombekere au Bugonoka nafasi ya kuhusiana na kujihusisha na mila na desturi za watu wake na hivyo kuwa mjumbe wa jamii hiyo.

Hitimisho

Katika makala haya tumeangalia nafasi ya riwaya ya *Bwana Myombekere*..... katika kutunza na kusambaza mila na desturi kwa watu wa jamii ya Wakerewe. Aidha tumegusia uwezekano wa usambazaji huo huvuka mipaka ya kabilia moja na kuwa mchango muhimu katika utamaduni wa Tanzania nzima. Makala haya yameonyesha kuwa kitabu hiki kimezingatia zaidi mila na desturi za Wakerewe kwa kutumia maisha ya kila siku ya familia ya Bwana Myombekere. Kwa kuyaangalia maisha hayo imewezezana kuuona uhusiano wa kimzunguko baina ya mtu, utamaduni unaomzunguka na muundo wa jamii yake na hivyo kuonyesha nafasi ya mila na desturi zilizozingatiwa na Kitereza zinavyotawala mtu. Hii imetokana na kuwa mila na desturi, japo zinatokana na watu, utamaduni na muundo wa jamii, zinakuwa na nguvu zaidi na kutawala vyote hivi. Makala haya vilevile yameonyesha njia zilizotumiwa na Kitereza, kwa makusudi au bila kujua, katika utunzaji na usambazaji mila na desturi hizo. Tumemalizia makala haya kwa kuangalia uhusiano baina ya mtu, mila na desturi na kuona kwamba kutokana na riwaya hii, mtu huwa na nafasi ndogo sana kuweza kusimama dhidi ya mila na desturi za jamii yake. Itokeapo akafanikiwa kufanya hivyo, basi huonekana kuwa nje ya hali zinazokubalika. Katika sehemu hii tumeangalia hali kadhaa za kiuhusiano zilizojitokeza katika kumfanya mtu aweze kuingizwa ndani ya mila na desturi za jamii.

Kwa kuzingatia haya yote, tutaona kuwa riwaya ya *Bwana Myombekere*..... ina muundo wa hali ya juu katika kujenga dhamira ya mila na desturi za Wakerewe. Muundo huu wa uhusiano wa kutegemeana unaifanya kila sehemu ya riwaya hii kuweza kujenga ukamilifu wa riwaya nzima.

MAREJE

- Anicet, A.O. na Wenzake (1979) *Utamaduni Chombo cha Maendeleo*. Wizara ya Utamaduni, Dar es Salaam.
- Ben-Amos, D.(1976) "The Concepts of Genre in Folklore" kwenye *Folklore Narrative Research*, Pentikainen, J. (Mhariri), SKS, Helsinki.
- Grim, J.(1934) *Teutomika Mythology*, London.
- Hartwig G. na Charlotte, M.(1972) "Anicet Kitereza: A Kerebe Novelist" RAL, vol.3 Texas.
- Kitereza, A.(1980), *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka*, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.
- Knappert, J.(1979). *Four Centuries of Swahili Verse*, Heinemann Educational Books Ltd., London.
- Langness, L.(1965). *Life History in Anthropological Science*, New York.
- Madumulla J.(1988). "Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka" *Kiswahili* 55, TUKI.
- Malinowski, B.(1973). *Theories of Man and Culture*, Hatch Elvin, New York.
- Mbiti, J.(1969). *African Religions and Philosophy*, r. Heinemann Educational Books, London.
- Mlacha, S.(1986). "Uprooting the Traditional Culture in Kiswahili Prose Fiction" kwenye *Africana Marbugensia* 2, Frankfurt.
- Mlacha, S.(1987), "Cultural Change as Portrayed in Kiswahili Prose? Fiction" kwenye *The Journal of Intercultural Studies*, Japan.
- Mlacha, S.(1987). The Potrayment of Cultural Conflict in Kiswahili Prose Fiction, tasnifu ya Ph.D London.
- Mlacha, S.(1996). "The Cultural Dimension in Swahili Novel" *Swahili Lit. Series*, London.

- Mulokozi, M.(1985). "A Kitereza: *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Ntulanalwa na Bulilwali*" kwenye Kiswahili 52/1 na 52/2, TUKI, Dar es Salaam.

Nenola-Kallio, A.(1986). "Folklore and Gender an Attempt at a Revision". Katika Jarvinen (Mhariri), *Contemporary Folklore and Culture Change*. Lansi - Oy, Finland.

Pentikainen, J.(1976). " Repertoire Analysis" katika *Folk Narrative Research*. SKS, Helsinki,

Sengo, T. na Lucas, S.(1975) *Utani na Jamii*. Foundation Books Ltd: Nairobi.

Von Sydow, C.(1948) "On the Spread of Tradition," katika Bodker L. (Mhariri), *Selected Papers On Folklore*. Copenhagen.